


# Matibabu ya Kingamaradhi ya Monoklonoli ni Nini?

---



Ukiwa katika hatari ya maradhi makali ya COVID-19 na umepatikana na maambukizo ya COVID-19 au umekuwa na mgusano wa karibu na mtu aliyeambukizwa, huenda ukataka kuzingatia matibabu ya kingamaradhi ya monoklonoli (mAb). Unaweza kufuzu kupata matibabu ya mAb ya kutibu COVID-19 kutegemea umri wako, historia ya afya, na kipindi ambacho umekuwa na dalili.

Matibabu ya mAb yanaweza kuzuia virusi vinavyosababisha COVID-19 kuingia kwenye seli za mwili wako na kupunguza kiwango cha virusi ndani ya mwili wako. Hii inamaanisha kuwa unaweza kuwa na hatari kiasi na unaweza kupunguza uwezekano wa wewe kuhitaji kukaa hospitalini.

Matibabu ya mAb yanaweza kuwasaidia watu ambao:

- Wapo katika hatari ya juu ya kupata dalili hatari zaidi **na**
- Kupatikana na maambukizo ya COVID-19 na dalili kukaa kwa siku **7** au kiasi **au**
- Wamekua katika mfiduo wa karibu na mtu aliyeapatikana na maambukizo hivi karibuni

---

## • KINGAMARADHI YA MONOKLONOLI NI NINI?

Mwili wako kiasili hutengeneza kingamaradhi za kupigana na maambukizo. Hata hivyo, mwili wako huenda usiwe na kingamaradhi zilizoundwa ili kutambua virusi vipya kama SARS-CoV-2, virusi vinavyosababisha COVID-19. Kingamaradhi za monoklonoli, au mAb, zinaundwa katika maabara ili kupigana na maambukizo maalum (kwa hali hii, SARS-CoV-2) na unapewa moja kwa moja kwa kudungwa. Matibabu ya mAb yanaweza kusaidia iwapo upo katika hatari ya juu ya dalili kali au kulazwa hospitalini.

Matibabu ya mAb ya COVID-19 ni tofauti na chanjo ya COVID-19. Chanjo hiyo huchochea mwitikio asili wa mwili wako, lakini hii inaweza kuchukua wiki ili kuwa na kingamaradhi ya kutosha kupigana na virusi. Hivyo, ukiwa na virusi, matibabu ya mAb hupatia mwili wako kingamaradhi inayohitaji kujilinda. Matibabu ya mAb hayachukui nafasi ya haja kingamwili ya chanjo lakini yanaweza kukusaidia ukiwa katika hatari ya kuwa na COVID-19 hatari.

## • JE, MATIBABU YA KINGAMARADHI YA MONOKLONOLI YANAWEZA KUFANYA NIWE MGONJWA?

Matibabu ya kingamaradhi hayana virusi vyovyote hai, hivyo hakuna hatari kuwa utapata COVID-19 kutokana na matibabu ya mAb. Hata hivyo, matibabu ya kingamaradhi yanaweza kuwa na

kingamwili. Tafadhali ongea na mhudumu wako wa afya kuhusu madhara yanayoweza kutokea na unachoweza kufanya ukiona dalili hizo kwako.

## • JE, NA IWAPO SITAFUZU KUPOKEA MATIBABU YA KINGAMARADHI YA MONOKLONALI?

Mhudumu wako wa afya anaweza kuamua kuwa hufuzu kupokea matibabu ya mAb. Huenda kuna sababu kadhaa kwa hili. Huenda usitimize vigezo vyote vya kustahiki, au huenda una hali iliyopo ya afya ambayohukufanya huenda usipokee matibabu ya mAb. Muulize mhudumu wako wa afya chaguo nyingine za matibabu.


## • JE, NAWEZAJE KUPATA KINGAMARADHI YA MONOKLONOLI?

Hatua ya 1: Kupatikana na maambukizo ya COVID-19 na kuwa na dalili kwa siku 7 au kiasi

Hatua ya 2: Pata rufaa kutoka kwa mhudumu wako wa afya.

Hatua ya 3: Tafuta kituo kinachopatikana.

Ili kupokea mAb unafaa kutumwa kupokea matibabu na mhudumu wako wa afya na kuelekezwa kwa vituo vinavyopatikana. **Iwapo huna mhudumu wa afya**, piga simu kwa Combat COVID Monoclonal Antibodies Call Center (Kituo cha Simu cha Kupigana na Kingamaradhi ya Monoklonoli) kupitia 1-877-332-6585 ili kupata mtu wa kuongea maye kuhusu dalili na matibabu yako.



DOH 825-031 March 2022 Swahili

Ili kuomba waraka huu katika muundo mwingine, piga simu 1-800-525-0127. Wateja ambao ni viziwi au wasio na uwezo wa kuzungumza, tafadhali piga simu 711 (Washington Relay) au tuma barua pepe kwa <mailto:ecivil.rights@doh.wa.gov>.